3. Anakili sentensi kisha apigie mstari vitenzi vifuatavyo: imewahakikishia. husafiria, kuwafulia, Tuliwapokelea, alimuinulia, kutobolea, alitumia, unampakulia, huichezea.

**Shughuli ya 2**

1. rudia, vulia, kopea, lelea, rarulia.
2. Mwanafunzi aandike sentensi upya. Vitenzi vilivyopigiwa mstari vigeuzwe na kuwa kama ifuatavyo: huombea, wananyunyizia, kuokotea, kutwangia, anahutubia.
3. Mwanafunzi atumie vitenzi alivyopewa kutunga sentensi.
4. Mwanafunzi atumie kifaa cha kidijitali kutunga sentensi. Atumie vitenzi alivyogeuza kwa kauli ya kutendea kama ifuatavyo: torokea, pulizia, katazia, fyekea, fikiria.

## C. Kauli ya kutendwa

**Shughuli ya 1**

1. Kauli ya kutendwa huonyesha hali ambapo jambo limefanywa na mtu au kitu, ai kitendo kimefanywa na mtu fulani.
2. Vitenzi katika kauli ya kutendwa katika jedwali ni: wazwa, amkuliwa, songwa, poswa, shikwa, laliwa, tembelewa, semwa, pigwa, pewa, chorwa.
3. Mwanafunzi anakili sentensi kisha apigie mstari vitenzi vifuatavyo: wamelipwa, litajengwa, kufuliwa, alipokelewa, aliyelazwa, imeondolewa, kushindwa, alinaswa, alishauriwa.

**Shughuli ya 2**

1. Majibu yanayotarajiwa: patwa, valiwa, kuzwa, imbwa, tolewa.
2. Mwanafunzi akamilishe sentensi. Vitenzi vilivyo mabanoni vigeuzwe na kuwa kama ifuatavyo: ombwa, ibwa, okotwa, limwa, bomolewa.
3. Mwanafunzi atumie vitenzi alivyopewa kutunga sentensi. Baadhi ya sentensi zihusu wanyama wa porini.
4. Mwanafunzi atunge sentensi. Atumie vitenzi alivyogeuza kwa kauli ya kutendwa kama ifuatavyo: chimbuliwa, endeshwa, olewa, futwa, kimbiwa.

## D. Kauli ya kutendewa

**Shughuli ya 1**

1. Kauli ya kutendewa huonyesha kwamba kitendo kilichofanywa kimeelekezwa kwa mtu mwingine.
2. Vitenzi katika kauli ya kutendewa katika skrini ni: vuliwa, songewa, ibiwa, shikiwa, tobolewa, jengewa, chorewa, somewa, chezewa.
3. Anakili sentensi kisha apigie mstari vitenzi vifuatavyo: wameshangiliwa, wamefuliwa, imeondolewa, huvuliwa, amejengewa, wameandikiwa, alikatiwa, Niling'olewa.

**Shughuli ya 2**

1. takiwa, tembelewa, fuatiwa, temewa,twaliwa.
2. Mwanafunzi akamilishe sentensi. Vitenzi vilivyo mabanoni vigeuzwe na kuwa kama ifuatavyo: pigiwa, andaliwa, somewa, achiwa, fungiwa.
3. Mwanafunzi atumie vitenzi alivyopewa kutunga sentensi.
4. Mwanafunzi atunge sentensi. Atumie vitenzi alivyogeuza kwa kauli ya kutendewa kama ifuatavyo: zibiwa, pokelewa, ombewa, kaziwa, kejeliwa.

## E. Kauli ya kutendeka

**Shughuli ya 1**

1. Kauli ya kutendeka huonyesha kwamba kitendo kimefanyika ila mtendaji hakudhihirika.
2. Vitenzi katika kauli ya kutendeka katika kapu maneno ni: kosekana, choteka, takikana, pigika, kalika, fumika, shikika, wezekana, teseka, bomoka, furika.
3. Anakili sentensi kisha apigie mstari vitenzi vifuatavyo: ukapikika, ilivunjika, wameerevuka, ulifungika, huchomeka, wameelimika, unateseka, hukatika.

**Shughuli ya 2**

1. lambika, mwagika, zoeleka, pimika, tambulika.
2. Mwanafunzi akamilishe sentensi. Vitenzi vilivyo mabanoni vigeuzwe na kuwa kama ifuatavyo: toboka, sambazika, tegeka, pendeka, vunjika.
3. Mwanafunzi atumie vitenzi alivyopewa kutunga sentensi.
4. Mwanafunzi atunge sentensi. Atumie vitenzi alivyogeuza kwa kauli ya kutendeka kama ifuatavyo: tumika, sikilizika, fuatika, chemshika, chomeka, fikirika.

## Shughuli jumuishi

1. (a) tambia, tambwa, tambiwa, tambika
   (b) vumia, vumwa, vumiwa, vumika
   (c) kerea, kerwa, kerewa, kereka
   (d) pakia, pakwa, pakiwa, pakika
   (e) kosea, koswa, kosewa, kosekana

2. (i) aliteseka – kauli ya kutendeka
   (ii) yamefurika – kauli ya kutendeka
   (iii) litachezewa – kauli ya kutendewa
   (iv) kumchapa – kauli ya kutenda
   (v) amefukuzwa – kauli ya kutendwa
   (vi) imezimika – kauli ya kutendeka
   (vii) wamehubiriwa – kauli ya kutendwa
   (viii) yamechimbwa – kauli ya kutendwa
   (ix) niliwapakulia – kauli ya kutendea
   (x) ametaga – kauli ya kutenda

## Shughuli ya kidijitali

Mwanafunzi atunge kifungu kifupi kuhusu ndege yoyote wa porini. Atumie kifaa cha kidijitali. Atumie vitenzi katika kauli mbalimbali katika kifungu hicho.

## F. Kauli ya kutendana

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   fichana, pakana, somana, chapana, nyoana,
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) kataana
   (b) toboana
   (c) sakana
   (d) lindana
   (e) chorana
3. Majibu yanayotarajiwa:

| Kitenzi | | Kutendana |
|---|---|---|
| a | tandika | tandikana |
| b | iba | ibana |
| c | angalia | angaliana |
| d | ruka | rukana |
| e | tazama | tazamana |

**Shughuli ya 2**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wabunge waliulizana maswali.
   (b) Watoto walichorana.
   (c) Ni vizuri kusaidiana wakati wa shida.
   (d) Kuchokozana ni kubaya.
   (e) Waridi na Zawadi walibebana mpaka nyumbani.
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Juma alibeba Maria naye Maria akambeba. Wote walibebana.
   (b) Nilimsaidia naye akanisaidia. Sote tulisaidiana.
   (c) Aliwakanyaga nao wakamkanyaga. Wote walikanyagana.
   (d) Ulimfukuza naye akakufukuza. Nyote mlifukuzana.
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia vitenzi alivyopewa. Kama hana kifaa cha kidijitali, aandike sentensi zake daftarini mwake. Mwanafunzi anaweza kujitathmini na wenzake.

## G. Kauli ya kutendeana

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   andikiana, kasirikiana, choreana, shambuliana.
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) pikiana
   (b) tikisiana
   (c) tembeleana
   (d) choreana
   (e) vunjiana
3. Majibu yanayotarajiwa:

| Kitenzi | | Kutendeana |
|---|---|---|
| a | inua | inuanaa_____________ |
| b | imba | imbiana |
| c | shona | shoneana_____________ |
| d | ruka | rukiana |
| e | rarua | raruana |

**Shughuli ya 2**

Majibu yanayotarajiwa:

(a) Wasomi wamejengeana majumba ya kifahari vijijini.
(b) Wanasiasa walichokozana siasani.
(c) Watoto huchekeana pekee yao majumbani.
(d) Wezi wameharibiana mipango yao mchana peupe.
(e) Wanasoka wanachezeana kabumbu kistadi.

## Shughuli ya kidijitali

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia vitenzi alivyopewa. Kama hana kifaa cha kidijitali, aandike sentensi zake daftarini mwake. Mwanafunzi anaweza kujitathmini na wenzake.

## H. Kauli ya kutendesha

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   lipiza, legeza, levya, chosha, ogofya

2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) chekesha
   (b) sahaulisha
   (c) toza
   (d) julisha/juvya
   (e) ogopesha/ogofya
3. Majibu yanayotarajiwa:

| Kitenzi | | Kutendesha |
|---|---|---|
| a | kata | katisha______ |
| b | fuata | fuatisha |
| c | lazimu______________ | lazimisha |
| d | penda | pendeza |
| e | kimbia | kimbiza |

## Shughuli ya 2

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wananchi ni sharti watozwe ushuru.
   (b) Majambazi wamefikishwa mahakamani
   (c) Fisi anamkimbiza sungura
   (d) Pombe hulevya.
   (e) Je, umewajuvya/juza habari hiyo?
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia vitenzi alivyopewa. Kama hana kifaa cha kidijitali, aandike sentensi zake daftarini mwake. Mwanafunzi anaweza kujitathmini na wenzake.

## I. Kauli ya kutendua

### Shughuli ya 1

1. Majibu yanayotarajiwa:
   fumbua, wazua, chimbua, fungua, kunjua, zibua,
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) fumua
   (b) chomoa
   (c) tundua
   (d) tegua
   (e) pakua

3. Majibu yanayotarajiwa:

| Kitenzi | | Kutendua |
|---|---|---|
| A | waza__________ | wazua |
| B | chimba | chimbua |
| C | tata__ | tatua |
| D | chana | chanua |
| E | remba | rembua |

**Shughuli ya 2**

Majibu yanayotarajiwa:

(a) Mafundi wanaezua nyumba ya jirani yangu.
(b) Wanafunzi walifumbua mafumbo ya mwalimu.
(c) Mawakili watafichua njama ya washukiwa.
(d) Askari alimfungua mhalifu pingu mikononi.
(e) Wametundua picha ya familia ukutani.

**Shughuli ya kidijitali**

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia vitenzi alivyopewa. Kama hana kifaa cha kidijitali, aandike sentensi zake daftarini mwake. Mwanafunzi anaweza kujitathmini na wenzake.

## 5. Vinyume vya Nomino

### A. Vinyume vya nomino

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) kijana
   (b) mkweli
   (c) mwenyeji
   (d) malkia
   (e) adui
2. Mwanafunzi atunge senetensi akizingatia nomino na kinyume chake sahihi.
   (a) tajiri – maskini
   (b) mfalme – malkia
   (c) rafiki – adui
   (d) jogoo – koo
   (e) mgeni – mwenyeji
   (f) binti – bin

**Shughuli ya 2**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) mwangaza – giza
   (b) kicheko – kilio
   (c) ardhi – mbingu
   (d) amani – vita
2. Mwanafunzi atunge sahihi akizingatia vinyume vya nomino zifuatazo:
   (a) utiifu
   (b) umoja
   (c) urafiki
   (d) kifo
   (e) udogo

**Shughuli ya 3**

1. Tumia rangi au kalamu yenye rangi mbalimbali kulinganisha mchoro na kinyume chake.
   (a) jogoo – koo
   (b) malkia – mfalme
   (c) ajuza – shaibu
   (d) huzuni – furaha
2. Andika kinyume cha sentensi hizi kwa kuzingatia maneno yaliyokolezwa rangi.
   (a) Tulikutana usiku. – Tulikutana mchana.
   (b) Huu ni mwanzo. – Huu ni mwisho.

(c) Nimepata baraka kutoka kwa wazazi wangu. – Nimepata laana /hizaya/apizo kutoka kwa wazazi wangu.
(d) Wauzaji walipata faida kubwa. – Wanunuzi walipata hasara kubwa.
(e) Wazee wanafaa kuwaheshimu wanawake. – Vijana wanafaa kuwaheshimu wanaume.
(f) Kuna kelele darasani. – Kuna kimya darasani.
(g) Nyumbani kwetu kuna kitwana mwema. – Nyumbani kwetu kuna kijakazi mwema.
(h) Nilikutana na marafiki wawili barabarani. – Nilikutana na maadui wawili barabarani.

3. Mama alimchinja koo Jumapili mchana. Wenyeji walikula wakashiba. Vijana waliketi mezani. Mama wa kambo aliketi karibu na halati yangu. Chakula kile kilipendwa na wenyeji wote. Wangapi wanapenda ukarimu?
4. Vinyume vya vitenzi vya kujaza nafasi:
   (a) joto
   (b) huzuni
   (c) Adui
   (d) ukweli
   (e) umaskini
   (f) nyuma
   (g) mwanzo
   (h) mamaye
5. Mraba – Tafuta kwenye mraba maneno haya.
   (a) mtawa – walii
   (b) kaka – dada
   (c) jogoo – koo
   (d) mwenyeji – mgeni
   (e) sakafu – paa
   (f) baba – mama
   (g) huzuni – furaha
   (h) mtanashati – mrembo
   (i) kimo – kina
   (j) jioni – asubuhi

## B. Vinyume vya vivumishi

### Shughuli ya 1

1. Daktari Kazikwisha ni mfupi kama Twiga. Ijapokuwa ni mkali, yeye ni maskini mdogo. Jina lake limevuma kama upepo wa kusi. Ana familia kubwa inayoishi mjini. Wafanyakazi wake wachache wanashughulikia majengo yake. Wafanyakazi hao wana mapokezi mabaya sana. Majengo yake yana miundo duni inayowavutia wageni wachache. Sijamwona mtu mbaya kama Kazikwisha.
2. Sentensi sahihi zizingatie vinyume vya maneno haya:
   (a) tamu – chungu/kali
   (b) mwoga – shujaa

(c) mweupe – mweusi
(d) mnene – mwembamba/mkondefu
(e) jepesi – zito
(f) mtiifu – mkaidi

3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Gari dogo limeanguka mtaroni.
   (b) Vijana wajinga watashikwa na polisi.
   (c) Njia ya mkweli ni ndefu.
   (d) Kisu kikali kitakata nyama kweli?
   (e) Nguo safi zitafuliwa na yaya.
4. Majibu yanayotarajiwa:
   Shule hii ina wanafunzi wengi sana.
   Vyakula vigumu huuzwa kwa bei nafuu.
   Mzigo niliobeba ni mwepesi sana.
   Matunda mabichi yanuzwa sokoni.
   Vijana hao ni karimu zaidi.
5. Majibu yanayotarajiwa:
   Dawa mbaya uliyoimeza ni chungu/ kali.
   Kijana mtiifu ndiye mwoga wetu.
   Sarara ni nyama laini kuliko maini.
   Mti mkomavu uliong'olewa umetupwa.
6. Vinyume vya vivumishi katika chati.
   **Kuteremka**
   mtulivu
   jeupe
   haba
   mkaidi
   shujaa
   bivu

   **Kulia**
   dhalili
   karimu
   safi
7. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Chumvi inauzwa kwa bei nafuu.
   (b) Mama amenunua maembe mabivu.
   (c) Kuna mahindi haba/machache nyumbani.
   (d) Mwanafunzi mkaidi/mtundu atafanya mtihani.
   (e) Jengo fupi limebomolewa.
   (f) James ni kiongozi mpole.
   (g) Ghorofa hiyo ina msingi dhaifu/mlegevu.

(h) Godoro jeupe limeanikwa.

## C. Vinyume vya vitenzi

**Shughuli ya 1**

1. Marisela ni mteja maarufu sokoni Marikiti. Siku moja, aliketi/ alikaa baada ya kumeza tembe zake hospitalini. Alielekea sokoni kuuza vyakula mbalimbali. Njiani, alikutana na wateja waliohuzunika/waliokasirika na kulia. Wazee walimlaani/walimwapiza na wengine pia wakamkashifu Marisela. Walimchukia kutokana na ukarimu wake. Alisimama akafungua mzigo wake akarudi nyumbani. Alipofika nyumbani, Marisela alimpata mama yake akianua nguo.
2. Mwanafunzi aigize kwa usahihi vitenzi alivyopewa.

**Shughuli ya 2**

Vinyume vya vitenzi katika jedwali

1. sahau – kumbuka
2. nunua – uza
3. lazimisha – ridhia
4. konda – nenepa
5. bariki – laani
6. tabasamu – nuna
7. pona – ugua

**Shughuli ya 3**

1. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia vinyume vya vitenzi alivyopewa katika hali ya kutendua. Tazama vitenzi vifuatavyo na vinyume vyake.
   (a) tega – tegua
   (b) vaa- vua
   (c) bana – banua
   (d) chana – chanua
   (e) ficha – fichua
   (f) ziba – zibua
   (g) pakua – pakia
   (h) shona – shonoa
   (i) tata – tatua
   (j) injika – injua/epua
2. Mwanafunzi atumie kifaa cha kidijitali kusakura ili kutambua vinyume vya vitenzi mbalimbali.

**Shughuli ya 4**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mwogeleaji amezama. – Mwogeleaji ameibuka.
   (b) Marashi yananuka. – Marashi yananukia.
   (c) Juma anajenga. – Juma anabomoa.
   (d) Maiti alizikwa. – Maiti alifukuliwa.
   (e) Mlango umefungwa. – Mlango umefunguliwa.
   (f) Mtoto anavaa nguo. – Mtoto anavua nguo.
2. Majibu yanayotarajiwa:
   Chumba kikifunguliwa, wafanyakazi wote watasimama sebuleni. Taa zote zitazimwa. Wenyeji watatoka na wapishi watawapakulia vyakula vya asili. Atakayechelewa kuingia atakosa nini? Lango kuu nalo litafunguliwa mapema kabla ya sherehe ya sikukuu kutia nanga.
   Bibiharusi atainuka na kulia kwa furaha. Bwana harusi ataufunua uso wa mke wake. Kila mmoja atawakemea maharusi kwa nderemo na shangwe. Wazazi nao watawakashifu.
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mwogeleaji aliibuka /alielea majini.
   (b) Ndege ya rais wa Kenya ilitua katika uwanja wa michezo.
   (c) Mwanafunzi huyu anakaidi maagizo ya walimu wake.
   (d) Sitakataa makosa yangu.
   (e) Nitausahau wema wako milele.
   (f) Wasichana wote wafumue nywele zao.
   (g) Tafadhali tufumbe macho tuombe.
   (h) Ng'ombe, mbuzi na ngamia wamenona sana.
4. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kinyume sahihi cha kitenzi mabanoni.
   (a) Wagonjwa wengo hospitalini wameugua.
   (b) Bwana Musa alimtaliki shangazi yangu.
   (c) Tulihamia mji wa Nairobi mapema mwaka huu.
   (d) Mkimbiaji Kipyegon anakashifiwa kwa ushindi wake.
   (e) Latifa anachukia sana kuuza peremende njiani.
5. Changamkia kutafuta vinyume katika mraba. Tumia rangi mbalimbali kuvibaini au kuvizingira kwa wino au mstari.
   (a) paa – tua
   (b) kusanya – tawanya
   (c) jenga – bomoa
   (d) zima – washa
   (e) tia – toa
   (f) kubali – kataa
   (g) tema – meza
   (h) nuka – nukia
   (i) taliki – oa
   (j) vaa – vua

### D. Vinyume katika hali ya kutendewa

**Shughuli ya 1**

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia vitenzi alivyopewa katika hali ya kutendewa. Tazama vitenzi vifuatavyo:

(a) pangiwa – panguliwa
(b) pikiwa – pakuliwa
(c) liliwa – chekewa/chekwa
(d) anikiwa – anuliwa
(e) dharauliwa – heshimiwa
(f) fungiwa – funguliwa

## 6. Nyakati na Hali

### A. Wakati uliopo (-na-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (b) wanavua
   (c) anapanda
   (d) anahubiri
   (e) wanasafisha
   (f) anajenga
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) anakimbia
   (b) anaandika
   (c) anatibiwa
   (d) analima
   (e) inatengenezwa
   (f) anafua
   (g) inapigwa
   (h) anaenda
   (i) anacheza
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (b) Nyanya anapika uji.
   (c) Dereva anaendesha gari jipya.
   (e) Mama anaosha mtoto kwa maji baridi.
   (f) Mwalimu anafundisha Kiswahili.
4. Majibu yanayotarajiwa (vitenzi katika wakati uliopo):
   (a) analisha
   (b) analinda
   (c) inasafishwa
   (d) kinapikwa
5. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Kwaya inaimba wimbo mzuri.
   (b) Baba anapika chai.
   (c) Wasoka wanacheza uwanjani.
   (d) Mama anaandika barua.
   (e) Kaka anafua chupi yake.
   (f) Mwanafuzi anacheka mwalimu akifundisha.

## B. Wakati uliopita (-li-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa (viambishi vya wakati uliopita):
   (a) alitupa
   (b) alikitengeneza
   (c) ilijengwa
   (d) alipalilia
   (e) alikitembelea
2. Majibu yanayotarajiwa (vitenzi katika wakati uliopita):
   (a) kilishonwa
   (b) tulipikiwa
   (c) zilifuliwa
   (d) ilisafishwa
   (e) waliuza
3. Majibu yanayotarajiwa (vitenzi katika wakati uliopita hali ya kuendelea):
   (b) zilikuwa zikishonwa
   (c) kilikuwa kiva
   (d) yalikuwa yakimwagika
   (e) ilikuwa ikiuzwa
4. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mwanafunzi alikuwa akichora dira.
   (b) Baba alikuwa akiandika barua.
   (c) Mama alikuwa akiosha mtoto kwa maji moto.
   (d) Wanafunzi walikuwa wakifagia darasa.
   (e) Mwalimu alikuwa akipangusa ubao.
   (f) Mtoto alikuwa akilala kitandani.

## C. Wakati ujao (-ta-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) litazuru
   (b) tutacheza
   (c) atawafunza
   (d) nitasoma
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) nitawajengea
   (b) atanipa
   (c) atampikia

(d) atatutembelea
(e) nitanunuliwa

3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) itakuwa ikiandikwa
   (b) itakuwa ikitengenezwa
   (c) litakuwa likilimwa
   (d) vitakuwa vikioshwa
4. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wanafunzi watalima shamba la shule.
   (b) Tutapanga safari yetu vizuri.
   (c) Kijakazi atamuosha mtoto.
   (d) Shangazi atatembea kwetu mwezi ujao.
   (e) Kesi hiyo itachunguzwa na afisa mkuu.

## D. Hali ya mazoea (hu-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) hutununulia
   (b) huwasaidia
   (c) huchukua
   (d) husoma
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) hutusimulia
   (b) huwasaidia
   (c) hutia
   (d) humwagika
   (e) hupenda
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Askari hulinda usalama wan chi.
   (b) Wanafunzi hurudi nyumbani kila siku.
   (c) Mtoto huamka akisikia kelele.
   (d) Yeye husikiliza walimu wake.
   (e) Mwanafunzi bora husaidia wenzake wakiwa na tatizo.
   (f) Baba hulima shamba lake kwa wakati ufaao.

## E. Hali timilifu (-me-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) limeondoka
   (b) imewasili
   (c) ameenda
   (d) amewatibu
   (e) amewatumbuiza
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) imezimika
   (b) imepotea
   (c) kimepatikana
   (d) amefika
   (e) ameanguka
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wanasoka wamecheza vizuri.
   (b) Baba amempiga mtoto.
   (c) Maji yamechotwa yakaisha.
   (d) Wageni wamefika shuleni mwetu.

## F. Hali ya masharti (-nge-, -ngali- na -ki-)

### 1. Hali ya masharti -nge-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) wangemaliza wangeenda
   (b) angevuna angeuza
   (c) angefika tungesoma
   (d) ningeosha ningepewa
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mwanafunzi angemaliza kazi angeenda kucheza.
   (b) Iwapo angetia bidii angepita mtihani huo.
   (c) Mzazi angefika mapema angempata mwalimu mkuu.
   (d) Mchezaji huyu angefuata maagizo angeepuka kuumia.

## 2. Hali ya masharti -ngali-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (b) ningalijua ningalimpata
   (c) ningalikuwa ningalimnunulia
   (d) ningalisoma ningalifaulu
   (e) tungalihudhuria tungalijifunza
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mama angalikuwa nyumbani angalifua nguo.
   (b) Angaliandika insha kwa hati nadhifu ingalisomeka.
   (c) Mtoto angalivua nguo zake zingalifuliwa mapema.
   (d) Angalisafisha vyombo vizuri angalipewa zawadi.

## 3. Hali ya masharti ya -ki-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) akipelekwa
   (b) akiwasaidia
   (c) wakifuata
   (d) ikijengwa
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wanafunzi wakicheza vizuri watatuzwa.
   (b) Wakulima wakipanda ipasavyo watavuna.
   (c) Mvua ikinyesha vizuri kutakuwa na mazao mengi.
   (d) Kazi ikiisha untaenda kucheza.
   (e) Mkisoma kwa bidi mtafaulu.
   (f) Mtoto akilala nitafua nguo zote.
   (g) Ukikimbia utamkuta mama dukani.
   (h) Ukiamka mapema hutachelewa kufika shuleni.

## Shughuli jumuishi

Wanafunzi washirikiane kufanya shughuli hii huku wakikosoana kwa heshima na upendo.

## 7. Ukanushaji

### A. Kiambishi cha nafsi na wakati ujao (-ta-)

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) **ha**wataomba
   (b) **ha**talima
   (c) **si**tamshirikisha
   (d) **ha**mtatuandikia
   (e) **hu**tanichora

### B. Kiambishi cha nafsi na wakati uliopo (-na-)

**Shughuli ya 2**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Sitaenda safarini.
   (b) Hajui kuimba.
   (c) Haandiki kwa kompyuta.
   (d) Hatupendi vyakula vya kiasili.
   (e) Hamkunywi maji safi.
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) utanifundisha
   (b) nitatumia
   (c) atalima
   (d) mtawekewa
   (e) tutaongozwa
   (f) watapatiwa
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Sitasahau
   (b) hawakukosa
   (c) sitaandika
   (d) Hutakosa
   (e) hapendi
   (f) hutaweza
   (g) hutaanguka
   (h) tusipige
   (i) sitapiga
4. Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutafuta maneno mbalimbali katika kompyuta na kutambua kwa usahihi viambishi vya nafsi na namna ya kuyakanusha.

5. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) cheza
   (b) nawa
   (c) lima
   (d) fagia
6. Majibu yanayotarajiwa:

| | Uyakinishi | Ukanushaji |
|---|---|---|
| (a) | Mtoto anacheza mpira. | Mtoto hachezi mpira. |
| (b) | Mimi ninapenda kuimba. | Mimi sipendi kuimba. |
| (c) | Wewe unatembea haraka. | Wewe hutembei haraka. |
| (d) | Yeye atakuja kesho. | Yeye hatakuja kesho. |
| (e) | Wanavuna mahindi shambani. | Hawavuni mahindi shambani. |

## C. Ukanushaji kwa kuzingatia viambishi vya wakati

### Shughuli ya 1

1. Majibu yanayotarajiwa:

| Nafsi | Kiambishi cha nafsi | Kiambishi cha wakati | Kikanushi |
|---|---|---|---|
| Kwanza umoja (mimi) | ni- | -li- (wakati uliopita) | siku- |
| Pili umoja (wewe) | u- | -ta- (wakati ujao) | huta- |
| Tatu umoja (yeye) | a- | -na- (wakati uliopo) | ha- |
| Kwanza wingi (sisi) | tu- | -na- (wakati uliopo) | hatu- |
| Pili wingi (nyinyi) | m- | -li- (wakati uliopita) | hamku- |
| Tatu wingi (wao) | wa- | -li- (wakati uliopita) | hawa- |

2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Juma **haku**ondoka shuleni mapema.
   (b) **Ham**tashirikiana kufanya kazi ya ziada.
   (c) **Si**jui kuchora wala kucheza zeze.
   (d) **Ha**imbi wimbo.
   (e) Sisi **hatu**takimbia uwanjani.
3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mimi sijui kucheza piano.
   (b) Wao hawakupigiwa simu na wazazi.
   (c) Sisi hatutafanya kazi za ziada.

(d) Mtoto hakumwimbia mwalimu wake.
(e) Hutanichorea mnyama mkubwa.

4. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Wanafundishwa kusoma na kuandika vizuri.
   (b) Ninapenda kutazama vibonzo nyumbani.
   (c) Alilima shamba lote.
   (d) Wao wanaelewa mchezo huo.
   (e) Wewe unajua kupika.
   (f) Mtaondoka asubuhi na mapema.
5. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) **si**takosa
   (b) **hawa**kujiunga
   (c) **huta**pata
   (d) **haku**funza
   (e) **hatu**takosa
6. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) **Si**takosa – Nafsi ya kwanza, umoja, wakati ujao
   (b) **Hawa**kujiunga – Nafsi ya tatu, wingi, wakati uliopita
   (c) **Huta**pata – Nafsi ya pili, umoja, wakati ujao
   (d) **Haku**funza – Nafsi ya pili, umoja, wakati uliopita
   (e) **Hatu**takosa – Nafsi ya kwanza, wingi, wakati ujao
7. Mwanafunzi asikilize makala au masimulizi katika kompyuta au simu ya mlezi au mzazi wake. Atambue sentensi na kuzikanusha akizingatia nafsi ya nyakati mbalimbali. Wanafunzi wanaweza kujitathmini na kukosoana kwa heshima na upendo.

## D. Ukanushaji wa viambishi vya masharti

### Hali ya masharti -ki-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   Nikichaguliwa – hali yakinishi
   Mkinipigia – hali yakinishi
   Wakijisajili – hali yakinishi
   Msiposhirikiana – ukanushaji
   Msiponipa – ukanushaji
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Ni**ki**mwona nitamsalimu. – Ni**sipo**mwona sitamsalimu.
   (b) U**ki**fanya bidii utapita mtihani wako. – U**sipo**fanya bidii hutapita mtihani wako.
   (c) Mwalimu a**ki**niona nitamjulia hali. – Mwalimu a**sipo**niona sitamjulia hali.

(d) Tu**ki**fika huko tutawaeleza mambo yote. – Tu**sipo**fika huko hatutawaeleza mambo yote.
(e) M**ki**cheza vizuri mtawashinda wapinzani. – M**sipo**cheza vizuri hamtawashinda wapinzani.
(f) Wa**ki**omba, msamaha wataupata. – Wa**sipo**omba, msahama hawataupata.

3. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Maji yasipojaa hayatamwagika.
   (b) Mtoto usipomlea vizuri hatafaulu.
   (c) Msipoingia darasani, hamtakutana na mwalimu Juma.
   (d) Walimu wasipoongezewa mshahara watagoma.
   (e) Sitakuona shule zisipofungwa.
   (f) Usiponiheshimu nami sitakuheshimu.
4. Mwanafunzi atunge sentensi tano sahihi akizingatia kiambishi -ki- cha hali ya masharti kisha azikanushe.
5. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Mkiziba ufa hamtajenga ufa.
   (b) Ukifuata maagizo ya daktari utapona.
   (c) Wakifika kituoni watapata magari.
   (d) Akisikia sauti yako ataamka.
   (e) Tukiwaheshimu walimu wetu hatutaangamia.

## Hali ya masharti -nge- na -ngali-

### Shughuli ya 1

1. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Msi**ngali**fundishwa vizuri msi**ngali**upita mtihani.
   (b) Wakimbiaji wa**nge**jiandaa vizuri wa**nge**shinda mbio hizo.
   (c) Wavuvi wa**nge**amka mapema wa**nge**pata samaki wengi.
   (d) Daktari asi**ngali**tumia dawa nzuri msi**ngali**pata matibabu bora.
   (e) U**nge**valia sare yako u**nge**ingia darasani.
2. Majibu yanayotarajiwa:
   (a) Usingefika hospitalini mapema usingempata daktari.
   (b) Tusingalisoma gazeti hilo tusingaliipata taarifa hiyo.
   (c) Nisingefuata maagizo ya mwalimu nisingeanguka mtihani wangu.
   (d) Asingalipata pesa asingalinunua simu.
   (e) Wasingetutumia ujumbe huo tusingejua habari hizo.
3. Majibu yanayotarajiwa (vitenzi vyenye viambishi vya masharti):
   tusi**ngali**fuata
   tu**ngali**umia
   a**nge**fuata
   asi**nge**angamia

wa**ngali**wasikiliza
wasi**ngali**lazwa
u**nge**kuwa
u**nge**fanya
tu**nge**zingatia
tu**nge**kuwa

4. Mwanafunzi atunge sentensi tano sahihi akizingatia kiambishi cha hali ya masharti -nge- kisha azikanushe kwa usahihi.
5. Mwanafunzi atunge sentensi tano sahihi akizingatia kiambishi cha hali ya masharti -ngali- kisha azikanushe kwa usahihi.

### Shughuli ya kidijitali

Mwanafunzi asakure katika kompyuta au simu ya mzazi au mlezi wake mifano ya sentensi mbalimbali zilizotumia viambishi vya hali ya masharti -nge- na -ngali-. Anakili sentensi hizi (nane) alizozitafuta katika kifaa cha kidijitali kisha awatumie wanafunzi wenzake mtandaoni ili wazisome na kuzitathmini usahihi wake. Wakosoane kwa heshima na upendo.

## 8. Ukubwa na Udogo wa Nomino Mbalimbali

### A. Ukubwa wa nomino zinazoanza kwa herufi 'm'

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   mji, mtu, mke na mbwa
2. Majibu yanayotarajiwa:
   jiji, jibwa, jito, jitu, jike na jijiwe
3. Majibu yanayotarajiwa:
   mto, mji, mke, mbwa na mtu
4. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kisarufi na kimantiki akitumia nomino alizopewa ambazo ziko katika hali ya ukubwa. Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Jibwa lilipatikana likila chakula jikoni.
   (b) Jitu hilo lilimkimbiza.
   (c) Jiji la Nairobi lina watu wengi.
   (d) Jike lake linaugua.
   (e) Jito hilo lina maji safi.

### Ukubwa wa nomino zinazoanza kwa herufi 'm' na zenye mzizi wa silabi mbili

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   mkate, mkono, mfupa, mkebe, mlango, mguu
2. Majibu yanayotarajiwa:
   kate, lango, koba, zee, lima
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya ukubwa. Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Kebe la asali limepotea.
   (b) Koba langu limenyeshewa.
   (c) Toto lile linalia kwa sauti.
   (d) Nilipewa fupa lililokuwa na nyama.
   (e) Lima lile ni ngumu kukwea.

### B. Ukubwa wa nomino zinazoanza kwa herufi 'n'

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   ndoo, ngamia, ndizi, ndege, ngoma, ngazi, ng'ombe

2. Majibu yanayotarajiwa:
   doo, zige, goma, dege, dama
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya ukubwa.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Dama lile linakimbia.
   (b) Gozi langu limekauka.
   (c) Doo la maji limepasuka.
   (d) Gazi lile limetumika kupandia mti.
   (e) Dege hilo lilipaa juu angani.
   (f) Guo lilishonwa na mama.

## C. Ukubwa wa nomino zinazoanza kwa kiambishi -ki-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kikapu, kiatu, kisu, kibuyu, kiazi, kikombe
2. Majibu yanayotarajiwa:
   jitabu, jiatu, jikiti, jitanda, jikombe
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya ukubwa.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Jisu langu limenikata.
   (b) Jisima lile limejaa maji.
   (c) Jichwa langu linauma.
   (d) Jipepeo lile lina rangi za kupendeza.
   (e) Jibuyu hili limejaa maziwa.

## D. Ukubwa wa nomino zinazoanza kwa kiambishi -ji-

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   jiwe, jimbi, jiko, jifya, jua, jina, jembe, jino
2. Majibu yanayotarajiwa:
   jijiwe, jijimbi, jijina, jijicho, jijibu, jijiko
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya ukubwa.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Jijimbi liliwika saa kumbi asubuhi.
   (b) Jijivu limetoka kwenye jijiko lile.
   (c) Aliambiwa ataje jijina lake.

(d) Jijiwe lile lilimwangukia mtoto.
(e) Jijino langu linahitaji dawa.

## E. Udogo wa nomino zinazoanza kwa herufi 'm'

### Udogo wa nomino zinazoanza kwa herufi 'm' na zenye mzizi wa silabi mbili

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kitoto, kilango, kiguu, kikoba, kikebe, kigongo, kisitu, kitaro
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya udogo.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Kilango kile kilivunjwa na wezi.
   (b) Kikono chake kilivunjika jana.
   (c) Kikebe cha asali kimepotea.
   (d) Kitoto kile kinalia kwa sauti.
   (e) Kisitu hicho kina Wanyama hatari.
   (f) Kidomo changu kinatoa damu.

### Udogo wa nomino zinazoanza kwa herufi 'm' na zina silabi moja.

Shughuli ya 1

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kijitu, kijibwa, kijito, kijiji
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya udogo.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Kijito hicho kina maji safi.
   (b) Kijiji cha Nairobi kina watu wengi.
   (c) Kijike chake ninaugua.
   (d) Kijibwa chake kilipatikana kikila chakula jikoni.

## F. Udogo wa nomino zinazoanza kwa herufi 'n'

**Shughuli ya 2**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kiguo, kizige, kigozi, kigoma, kidama
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya udogo.
   Majibu yanayopendekezwa:

(a) Kiguo kilishonwa na mama.
(b) Kidoo kimejaa maji.
(c) Kiguzo hicho ni imara.
(d) Kidoto hicho kilinishangaza.
(e) Kidama kile kinacheza.

## G. Udogo wa nomino zinazoanza kwa kiambishi 'ki'

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kijikombe, kijiatu, kijipepeo, kijitanda, kijitabu
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya udogo.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Kijipepeo kile kina rangi za kupendeza.
   (b) Kijitabu chake kimepotea.
   (c) Kijiazi hiki kimeiva.
   (d) Kijisu changu kimenikata.
   (e) Kijifuniko hiki ni cha kitoto kile.
   (f) Kijikapu hiki kimejaa matunda.
   (g) Kijisima kile kimejaa maji.

## H. Udogo wa nomino zinazoanza kwa kiambishi 'ji'

**Shughuli ya 1**

1. Majibu yanayotarajiwa:
   kijijivu, kijijiko, kijijifya, kijijicho, kijijiwe
2. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia nomino alizopewa zilizo katika hali ya udogo.
   Majibu yanayopendekezwa:
   (a) Kijijiwe kile kilianguka vibaya.
   (b) Kijijivu kimemwagwa chote.
   (c) Kijijina chake kinachekesha.
   (d) Kijijimbi kiliwika mapema leo.
   (e) Kijijino chake kitang'olewa na daktari.
   (f) Kijijimbo hicho kina watu wengi.

**Shughuli ya 2**

1. Jibu linalotarajiwa:
   (c) Zee limepigwa na majizi.
2. Jibu linalotarajiwa:
   (d) Gombe litachinjwa leo.